
Jarida La

# MIFUGO NA UVUVI

TOLEO NO; WMU 014| 2026 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

## *Serikali na IFAD kushirikiana mageuzi ya sekta za mifugo na uvuvi*




*Januari 2026*

Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni

HALIUZWI

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Yaliyomo


1 Bodi ya Uhariri.............Uk. 04

2 Serikali na IFAD kushirikiana mageuzi ya sekta za mifugo na uvuvi............Uk. 05

3 Kamani ainadi mamlaka ya uvuvi bungeni.......Uk 06

4 Wakuzaji viumbe maji 2,000 kufundishwa ufugaji bora wa samaki .Uk. 07

5 Wabunge wapigwa msasa kuhusu sekta za mifugo na uvuvi.......... Uk. 08

6 Wanawake TAWFA waanza kupata neema, serikali yatoa neno... Uk. 09

7 Matukio katika picha .. UK. 10

8 VCT yasajili wataalam wa mifugo 293 wenye sifa stahiki ........Uk. 11

9 TADB yaagiwa kuongeza wigo mikopo ya wafugaji, wavuvi ..... Uk. 12

10 Serikali yaanza kutenga maeneo ya malisho kwa wafugaji.... Uk. 13

11 Dkt. Bashiru akutana na Mwakilishi Mkazi wa FAO......... Uk. 14

12 Badilisheni hatilimiliki ya kiwanja cha ujenzi wa taasisi - Dkt. Bashiru....Uk. 15

13 BBT yatakiwa kuwekeza kwenye kuzalisha malisho ya mifugo........Uk. 16

14 Matukio katika picha........Uk. 17

15 Matangazo.......Uk. 18
















# Bodi ya Wahariri:

**Mwenyekiti**
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mhariri**
**Edward Kondela -** Afisa Habari Mwandamizi

**Msanifu**
**Hamisi Hussein** - Afisa Habari

**Wajumbe**
**Elibariki Mafole -** Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike -** Afisa Habari Mwandamizi
**Stanlay Bryaton -** Afisa Habari
**Chiku Makwai-** Afisa Habari
**Martha Mbena** - Afisa Habari
**Fausta Njelekela** - Afisa Habari

# Serikali na IFAD kushirikiana mageuzi ya sekta za mifugo na uvuvi

## Na, Hamis Hussein

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa (Mb.), amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) ambapo wamejadili kuhusu miradi inayotekelezwa kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika Januari 16, 2026, ofisini kwake Mtumba, jijini Dodoma, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ameonesha kufurahishwa na ujio wa ujumbe huoikiwanisehemuyakutambua mchango wa IFAD nchini.

Amesema serikali ya awamu ya sita imeendelea kuimarisha mazingira rafiki ili kuruhusu wawekezaji na sekta binafsi kushiriki katika kusukuma maendeleo ya wananchi.

Ujumbe huo wa IFAD umeongozwa na Mkurugenzi wa Nchi na Mwakilishi wake nchini Tanzania, Bw. Seth Meng pamoja na Mratibu wa Mpango wa Nchi wa IFAD, Bi. Jacqueline Machangu.

Majadiliano hayo yalijikita kujadili mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP) na Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inayotekelezwa kati ya sekta ya mifugo na uvuvi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa (Wa kwanza kushoto) akizungumza na Ujumbe wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) nchini Tanzania kujadili miradi inayotekelezwa katika sekta za mifugo na uvuvi, wakati wa kikao kilichofanyika ofisini kwake Januari 16, 2026 Mtumba, Jijini Dodoma.



# KAMANI AINADI MAMLAKA YA UVUVI BUNGENI



## Wakati akijibu hoja za wabunge katika kipindi cha maswali na majibu

**Na,Omary Mtamike**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Ng'wasi Kamani amelieleza bunge kuwa katika kukabiliana na changamoto ya Uvuvi usiofuata sheria serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi itakayofanikisha kudhibiti changamoto kwenye maeneo yote ya uvuvi nchini.

Mhe. Kamani amesema hayo Januari 27, 2026 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma wakati akijibu maswali ya wabunge mbalimbali waliotaka kufahamu hatua ambazo serikali imechukua katika kudhibiti vitendo vya uvuvi usiofuta sheria ambapo amesema kuwa hatua hiyo itarahisisha utekelezaji wa mpango kabambe wa sekta ya Uvuvi wa mwaka 2021-2037 wenye kipumbele cha kuanzisha, kufufua, kuendeleza na kuimarisha viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi nchini.

"Mhe. Spika ili kuhakikisha viwanda vyetu vinafanya kazi kulingana na matarajio ya serikali, wizara ipo katika hatua za maamuzi kulingana na taratibu za serikali za kuanzisha mamlaka ya uvuvi kwa lengo la usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kupambana na uvuvi usiozingatia sheria." Amesema Mhe. Kamani.



Aidha, Mhe. Kamani amebainisha hatua za awali ambazo wizara imezitekeleza ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa malighafi ya samaki ikiwa ni pamoja na kuweka maboya 32 yenye thamani ya shilingi milioni 224 katika eneo la Uchelele mkoani Mwanza. Mhe. Kamani ameongeza kuwa wizara imeendelea kuhamasisha ufugaji samaki kwa njia ya vizimba ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa samaki na kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi kwenye viwanda.

Akijibu swali linalohusiana na mikakati ya serikali kwenye ujenzi wa viwanda vya nyama, Mhe. Kamani alisema kuwa wizara inaendelea kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili wawekeze kwenye eneo hilo huku pia akisisitiza kuendelea kuhamasisha wafugaji wote nchini kufuga kisasa ili viwanda hivyo viweze kupata mazao yenye ubora.

# WAKUZAJI VIUMBE MAJI 2000 KUFUNDISHWA UFUGAJI BORA WA SAMAKI



**Na, Stanley Brayton**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP), ikiwa na lengo la kuwajengea uwezo wakuzaji viumbemaji katika uzalishaji wa samaki, kutengeneza chakula cha samaki, usimamizi wa mabwawa na masuala ya jinsia na lishe ili kuimarisha mifumo jumuishi ya usalama wa chakula.

Akizungumza katika kikao kazi cha kutekeleza programu hiyo Januari 15, 2026 wilayani Songea mkoani Ruvuma, Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mali ambaye alimuwakilisha Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Bw. Deogratius Sibula amesema programu ya (AFDP) inayotekelezwa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni nyenzo muhimu ya serikali katika kuimarisha sekta ya ukuzaji viumbemaji nchini.

"Programu hii itafanyika katika halmashauri tano za Mkoa wa Ruvuma ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Halmashauri za Wilaya ya Mbiga, Namtumbo, Nyasa na Tunduru," amesema Bw. Sibula

Aidha, Bw. Sibula amesema kuwa utekelezaji wa majukumu ya programu hiyo inalenga kutoa mafunzo kwa wakuzaji viumbemaji 2,000 katika Mkoa wa Ruvuma ambapo katika awamu hii utafanyika katika kata 25 ndani ya Halmashauri hizo 5 za Mkoa wa Ruvuma, kuanzia tarehe 15 Januari 2026 hadi tarehe 22 Januari 2026.

Vilevile, Bw. Sibula amebainisha kuwa mafunzo haya ni fursa kwa wakuzaji viumbe maji na yatakuwa na tija kubwa kwa wafugaji wa samaki wa mkoani Ruvuma na kuhamsha hali ya ufugaji kutoka ule wa kujikimu na kuwa na ufugaji wa kibiashara unaozingatia mbinu bora za ufugaji.

Kwa Upande wake, Afisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambaye ni Afisa Kiungo wa Programu ya AFDP, Bi. Mkomanile Mahundi amesema zoezi hilo litajumuisha wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu (PMO) pamoja na wataalam kutoka Halmashauri nane za mkoa wa Ruvuma.

Bi. Mahundi amebainisha kuwa mafunzo hayo ni endelevu na yataendelea kutolewa katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Morogoro, Tanga, Geita pamoja na Mkoa wa Tabora. wa zoezi la chanjo na utambuzi wa mifugo kitaifa ili kuongeza wigo wa kuwafikia wafugaji wengi zaidi.

Katika maeneo mbalimbali ya ziara yake, Mhe. Naibu Waziri Kamani amepokea maoni ya wananchi hususan wafugaji kuhusu changamoto ya upatikanaji wa maji ya kutosha, majosho na mbegu za malisho huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto hizo kwa kushirikiana na wananchi.



Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo wakiwa kwenye semina kuhusu majukumu na maendeleo ya sekta ya mifugo na uvuvi iliyofanyika Januari 19 na 20, 2026 bungeni jijini Dodoma.

# Wabunge wapigwa msasa kuhusu sekta za mifugo na uvuvi

**Na, Chiku Makwai, Hamisi Hussein**

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo wamepewa semina kuhusu majukumu mbalimbali yanayofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Taasisi zake.

Semina hiyo ya siku 2 imefanyika Januari 19 na 20, 2026 Bungeni Jijini Dodoma ambapo mara baada ya kupewa semina hiyo wajumbe hao walitoa maelekezo mbalimbali ikiwemo kuharakisha mchakato wa kuunda Mamlaka ya Uvuvi nchini ili kusaidia usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kuongeza tija ya kiuchumi na usalama wa chakula kupitia uzalishaji wa malisho ya mifugo.

Kamati hiyo inayongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Deudatus Mwanyika, baada ya semina kutoka kwa wataalam wa wizara hiyo alitoa maagizo kwa niaba ya kamati kuhusu mchakato wa mamlaka ya uvuvi na upatikanaji wa malisho ya mifugo.

“Pamoja na jitihada hizo, lakini tunaomba huu mchakato wa kuunda mamlaka ya uvuvi uharakishwe kwa sababu usimamizi wa uvuvi bado unachangamoto, vilevile suala la malisho liangalieni “alisema Mhe. Mwanyika.

Akitolea ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizoibuliwa na wajumbe wa kamati hiyo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amesema wizara inaendelea kuimarisha sekta ya uvuvi kwa kujenga bandari ya uvuvi ambayo ujenzi wake umefikia asimia 90 na mkandarasi anatarajiwa kukabidhi bandari hiyo ifikapo Machi 31 mwaka huu.

Balozi Dkt. Bashiru amesema baada ya kukamilika kwa bandari hiyo, serikali itanunua meli mbili kwa ajili ya shughuli za uvuvi wa bahari kuu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa lengo la serikali la kuwa na meli tano za uvuvi.

Semina hiyo iliyolenga kuliongezea bunge uelewa kuhusu shughuli zinazofanywa na sekta za mifugo na uvuvi na mabadiliko yanayotarajiwa katika sekta hizo. Semina hiyo imefanyika siku mbili Januari 19 na 20,2026 katika Viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

# Wanawake TAWFA waanza kupata neema, Serikali yatoa neno



Picha ya pamoja ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, watendaji wa Wizara na viongozi wa TAWFA baada ya kikao cha kujadili maendeleo ya wanawake katika sekta ya mifugo na uvuvi Januari 22, 2026 Mtumba Jijini Dodoma.

## Na, Fausta Njelekela

Jukwaa la Wanawake wanaojishughulisha na Uvuvi Tanzania (TAWFA), limekutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Meena, jijini Dodoma Januari 22, 2026 kwa lengo la kuishukuru serikali na kueleza mafanikio waliyopata wanawake hao tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019.

Akiwasilisha taarifa ya jukwaa hilo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mwenyekiti Jukwaa la Wanawake wanaojishughulisha na Uuvi Tanzania (TAWFA), Bi. Beatrice Mmbaga alisema TAWFA imefanikiwa kuanzisha kanda mbalimbali ikiwemo Kanda ya Maji ya Bahari na Pwani, Kanda ya Ziwa Tanganyika, Kanda ya Ziwa Victoria pamoja na Kanda ya Ziwa Nyasa na Maji Madogo huku akifafanua kuwa hatua hiyo imeongeza ushiriki wa wanawake, upatikanaji wa mitaji, elimu na vitendea kazi.

“Zaidi ya wanawake 2000 wa TAWFA wamefaidika na VICOBA kwa kupata mikopo yenye riba nafuu yenye thamani zaidi ya shilingi 160,000,000, huku TAWFA ikiendelea kuimarika kwa kutambulika kikanda na kimataifa ambapo sasa ni mwanachama wa World FisherFolks na African Women FishWorkers Association (AWFISHNET),” alibainisha Bi. Mmbaga.

Bi. Mmbaga alisema vipaumbele vyao mbalimbali ni kupata ithibati ya ubora ya TBS ili waweze kusafirisha bidhaa zao nje ya nchi, upatikanaji wa vitambulisho, kuwaunganisha wanachama wao na taasisi za kifedha pamoja na Masoko ya Nje na kuwawezesha wanachama mafunzo ya uongozi na elimu ya namna ya kuendesha vikundi vyao huku wakiiomba wizara kuwasaidia vitendea kazi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agness Meena baada ya kusilikiliza taarifa hiyo, aliwaeleza kuwa wizara kama mlezi wao itaendelea kushirikiana na TAWFA kwa kuwaunganisha na taasisi mbalimbali za kifedha pamoja na benki, hatua itakayowasaidia wanachama wa chama hicho kupata mikopo na mitaji kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi.

Aidha, Bi. Meena aliwahimiza viongozi hao wa TAWFA kuendelea kujiimarisha zaidi kwa lengo la kuweka misingi mizuri ya kujitegemea zaidi kiuchumi na kukuza shughuli zao ili kuimarisha mchango wa wanawake katika sekta ya uvuvi nchini huku akiwahimiza kuanzisha vyama vya ushirika vya kifedha (SACCOS) ili kuwawezesha wanachama kupata mitaji.

Awali, Mwakilishi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Bi. Prisca Issangya alieleza kuwa lengo la FAO ni kuinua wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata elimu na uwezo huku akiendelea kubainisha kuwa FAO iko tayari kushirikiana na TAWFA katika kuwaunganisha wanawake na mashirika ya fedha ili kuwasaidia kupata rasilimali zitakazowawezesha kukuza shughuli zao.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Semina ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu shughuli zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyofanyika Januari 19 na 20, 2026.













# VCT YASAJILI WATAALAM WA MIFUGO 293 WENYE SIFA STAHIKI

**Na, Stanley Brayton**

Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) limekamilisha mapitio na kusajili Wataalam wa Wanyama wenye sifa stahiki, pamoja na kusajili vituo mbalimbali vya kutoa Huduma za Afya ya Wanyama, ikiwa ni moja ya utekelezaji wa Sheria ya Veterinari SURA 319.

Akizungumza katika Kikao cha 62 cha Baraza cha kujadili utekelezaji wa shughuli za baraza hilo kwa robo ya pili ya mwaka wa 2025/2026, Januari 27, 2026 jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari Tanzania (VCT), Prof. Lughano Kusiluka amesema baraza limepitia na kuridhia kuwapa usajili watoa Huduma za Afya ya Wanyama 293 na Vituo 130 vya utoaji Huduma za Afya ya Wanyama.

"Usajili huu umefanyika kwa kuzingatia Sheria ya Veterinari SURA 319, kwa kuangalia vigezo mbalimbali stahiki." amesema Prof. Kusiluka

Aidha, Prof. Kusiluka amewataka wataalam hao na vituo hivyo kutoa huduma hizo kwa uweledi na utaalam kwa wafugaji kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi katika kutoa huduma hizo ambazo zimewekwa katika Sheria ya Veterinari.

Vilevile, Prof. Kusiluka amewataka wafugaji kuwatumia wataalam hao ambao wamesajiliwa na baraza kwa kufuata sheria ili kuepukana na athari ambazo zinaweza kuleta madhara katika mifugo yao, yatokanayo na wataalam wasiosajiliwa.

Kwa upande wake, Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania (VCT) ambaye pia ni Katibu wa baraza hilo, Dkt. Amani Kilemile amesema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Waziri wake mwenye dhamana, Mhe. Bashiru Ally Kakurwa inaendelea kuhakikisha kuwa wafugaji na mifugo wanapata huduma bora ambayo inatolewa na wataalam ambao wamethibitishwa na kupewa usajili pamoja na leseni kutoka mamlaka husika.



# TADB yaagizwa kuongeza wigo mikopo ya wafugaji, wavuvi



## Dkt. Bashiru akiimwagia sifa kuwa mshirika wa maendeleo

**Na, Hamisi Hussein**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amekutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TABD) na kufanya mazungumzo yanayolenga kuendeleza ushirikiano kati ya wizara na benki hiyo na kuitaka kuendeleza miradi ya sekta za mifugo na uvuvi.

Mazungumzo hayo yamefanyika Januari 27, 2026 katika ofisi ndogo ya wizara hiyo iliyopo Kambarage Tower Jijini Dodoma, ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TADB alifika kujitambulisha kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kuimarisha ushirikiano katika kuendeleza sekta za Mifugo na Uvuvi.

Katika Mazungumzo hayo, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ameipongeza Benki ya TADB kwa jinsi inavyoshirikiana na wizara na kuiagiza kupanua wigo wa kuwasaidia wafugaji wadogo kupata mikopo nafuu ili waweze kuendeleza miradi yao, pamoja na kuongeza ushiriki wa taasisi za kifedha kupitia TADB katika kutoa mikopo kwenye sekta za mifugo na uvuvi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Bw. Frank Nyabundege amempongeza Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa kwa kuteuliwa kuwa mbunge na Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kuahidi kuongeza kasi ya utoaji mikopo kwenye sekta ya mifugo na uvuvi hasa kwenye miradi inayowalenga vijana na wanawake.

Aidha, Bw. Nyabundege aliwasilisha taarifa fupi kuhusu ushiriki wa TADB katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi nchini ambapo kupitia TADB kama Benki ya Kisera inashirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuleta maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi ikiwem Benki kutoa mikopo ya mradi wa boti, ufugaji samaki kwa njia ya vizimba na mikopo ya vijana kupitia Programu ya BBT mifugo.

Kupitia mikopo ya miradi ya boti na vizimba TADB ilipokea kiasi cha Shilingi Bilioni 34.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi ambapo hadi sasa kiasi cha Shilingi Bilioni 29.83 kimetolewa kwa wanufaika 5,932 katika mikoa 16 hapa nchini.

Aidha, TADB kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanikiwa kutoa jumla ya boti 219 na vizimba 536 kwa wanufaika wa miradi. Aidha, kwa kupitia mradi wa vijana wa BBT Mifugo, kiasi cha Shilingi Milioni 847.3 kimetolewa kwa wanufaika 106 kwa miradi ya mikopo isiyo na riba.

Bw. Nyabundege aliongezea kuwa TADB imewasilisha ushiriki wake katika kutoa mikopo katika sekta ndogo ya maziwa nchini kupitia mradi wake wa TI3P ambapo kiasi cha shilingi bilioni 40 kimetolewa kwa wafugaji na wasindikaji wa maziwa nchini. Aidha, kupitia mradi wa TI3P TADB imefanikiwa kurekebisha na kujenga vituo 23 vya kukusanya maziwa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 1.1 kwa kushirikiana wafugaji, wizara, Halmashauri na wasindikaji wa maziwa.

# Serikali yaanza kutenga maeneo ya malisho kwa wafugaji

Kamani aeleza mikakati ya serikali, Jumla ya hekta milioni 2.51 kutumiwa na wafugaji


**Na, Hamisi Hussein**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza kutekeleza mkakati wa miaka mitano wa kuongeza maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji kwa kutenga hekta milioni 2.51, ikiwa ni sehemu ya kuongeza maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa shughuli za ufugaji kutoka hekta milioni 3.49 hadi hekta milioni sita.

Kauli hiyo ya serikali imetolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Ng'wasi Kamani Januari 28, 2026 Bungeni Jijini Dodoma wakati akijibu Swali la Mbunge wa Ngorongoro, Mhe. Yannick Ikae Ndoyinyo lililohoji serikali inampango gani wa kuongeza maeneo ya malisho kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inavyosema?

"Mhe. Spika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wizara, idara na taasisi zenye majukumu ya kisheria ya kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi tumeanza kuandaa mkakati wa miaka mitano wa kutenga hekta milioni 2.51 kwa ajili ya shughuli za ufugaji, wakati wa utekelezaji wa mkakati huu waheshimiwa wabunge wote watashirikishwa" alisema Mhe. Kamani.

Aidha, Mhe. Kamani amesema wizara itaendelea kutoa taarifa na elimu kwa wafugaji kote nchini kupitia vyombo vya habari kuhusu mabadiliko ya tabianchi ili kuwasaidia wafugaji kuchukua tahadhari ya kuikinga mifugo yao, pia katika kutafuta unafuu wa changamoto ya malisho serikali imeshusha bei ya mbegu za malisho kutoka shilingi 4,000 kwa kilo hadi shilingi 1,000.





***"Mhe. Spika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wizara, idara na taasisi zenye majukumu ya kisheria ya kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi tumeanza kuandaa mkakati wa miaka mitano wa kutenga hekta milioni 2.51 kwa ajili ya shughuli za ufugaji, wakati wa utekelezaji wa mkakati huu waheshimiwa wabunge wote watashirikishwa***

# Dkt. Bashiru akutana na Mwakilishi Mkazi wa FAO

## Na, Hamis Hussein

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amekutana na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) Nchini Tanzania, Dkt. Nyabenyi Tipo na kufanya mazungumzo yanayolenga kuendeleza ushirikiano katika kukuza na kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

Kikao hicho kimefanyika Januari 29, 2026 katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo Kambarage Tower Jijini Dodoma ambapo Mhe. Balozi Dkt. Bashiru amesema serikali ya awamu ya sita imetoa kipaumbele kwenye bajeti kwa sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi.

Hivyo juhudi zinazofanywa na FAO katika sekta za uzalishaji ni ishara ya kuimarisha uchumi wa wananchi, na kumhakikishia Dkt. Tipo kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na FAO zitaendelea kushirikiana katika kuendeleza sekta hiyo ili kuimarisha uchumi wa wananchi na usalama wa chakula.

Naye, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) Nchini Tanzania, Dkt. Nyabenyi Tipo amesema Tanzania imendelea kupiga hatua katika kuchangia ukuaji wa pato la taifa kupitia sekta za uzalishaji na kwamba FAO itaendelea kutoa ushirikano ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa kutoka asilimia 5 ya sasa hadi kufikia asilimia 6.5 katika mwaka unakuja.

FAO imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiwemo udhibiti wa magonjwa kupitia mpango wa utoaji chanjo, miradi ya ukuzaji viumbe maji pamoja na uwezeshaji wa wafugaji na wavuvi kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula.

Mwakilishi Mkazi wa FAO nchini Tanzania Dkt. Tipo ametumia nafasi hiyo, pia kujitambulisha na kumpongeza Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kukurwa kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa (Wa kwanza kushoto) akizungumza na Ujumbe wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) nchini Tanzania kujadili miradi inayotekelezwa katika sekta za mifugo na uvuvi, wakati wa kikao kilichofanyika ofisini kwake Januari 16, 2026 Mtumba, Jijini Dodoma.

# Badilisheni hatimiliki ya kiwanja cha ujenzi wa taasisi - Dkt. Bashiru



## Na, Omary Mtamike

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, ameagiza kubadilishwa kwa hati miliki ya kiwanja kinachotumika kwenye mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya taasisi sita zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Balozi Dkt. Bashiru ametoa agizo hilo Januari 13, 2026 wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaotekelezwa eneo la Njedengwa jijini Dodoma ambapo amesisitiza kuwa hatua hiyo ni muhimu kiutawala na kisheria na itahakikisha umiliki halali wa mali ya serikali na kuwezesha matumizi endelevu ya jengo hilo mara baada ya kukamilika.

Balozi Dkt. Kakurwa amesema kuwa jengo hilo linajengwa kwa lengo la kuzikutanisha taasisi hizo ili kuboresha uratibu wa shughuli za kiutendaji, kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi zilizokuwa zikitumika maeneo tofauti.

“Ni lazima taratibu zote za umiliki wa ardhi zikamilishwe kwa wakati ili kuepusha changamoto za kisheria na kiutendaji hapo baadaye na hati ya kiwanja hiki inapaswa kuwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ili kuwezesha usimamizi mzuri wa mradi na jengo lenyewe,” amesema Balozi Dkt. Bashiru

Aidha, Balozi Dkt. Bashiru amewataka wasimamizi wa mradi na wakandarasi kuhakikisha wanazingatia viwango vya ubora, thamani ya fedha na ratiba ya utekelezaji kama ilivyoainishwa kwenye mkataba huku akisisitiza kuwa serikali haina nia ya kuona miradi ya maendeleo ikikwama kutokana na uzembe au kutokamilisha taratibu muhimu ambapo amemtaka Mshauri Mwelekezi wa mradi huo ambaye ni Wakala wa Majengo nchini (TBA) kuhakikisha anapitisha vibali vyote muhimu kwa haraka ili kuepuka kuchelewesha kukamilika kwa mradi huo.

Kwa upande wao, viongozi na wataalamu wa Wizara hiyo wamekiri kupokea maelekezo hayo ambapo wameahidi kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo kwa kufuata taratibu zote za kisheria, sambamba na kuendelea kusimamia utekelezaji wa ujenzi huo ili kukamilika kwa wakati uliopangwa.

Mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya taasisi sita zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi unaotarajiwa kutumia zaidi ya Tshs. Bilioni 49 ni miongoni mwa miradi ya kimkakati inayolenga kuimarisha utendaji wa wizara, kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma na kuchochea maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi nchini.



*Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa (wa pili kushoto) akizungumza na wakuu wa taasisi za wizara hiyo wakati akikagua mradi wa ujenzi ofisi za makao makuu ya taasisi hizo, eneo la Njedengwa jijini Dodoma Januari 13, 2026.*



# BBT yatakiwa kuwekeza kwenye kuzalisha malisho ya mifugo

**Na, Hamis Hussein**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa amezitaka taasisi zinazotekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) kutumia maeneo yao kuzalisha malisho ya mifugo ili kuimarisha ufugaji wa kibiashara.

Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa ametoa kauli hiyo Januari 31, 2026 alipokagua kituo cha BBT cha unenepeshaji wa mbuzi na kondoo Kongwa mkoani Dodoma, akizitaka Kampuni za Ranchi ya Taifa (NARCO), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuweka kipaumbele katika uzalishaji wa malisho kibiashara, kutokana na kwamba taasisi hizo zina ardhi, utaalam na uzoefu wa kutosha kufanikisha azma hiyo.

"Vituo vyetu vyote vyenye ardhi kubwa kama hizi TALIRI, NARCO, LITA kwa sababu tuna utaalam na uzoefu mkubwa nguvu zote zipelekwe kwenye uzalishaji wa malisho, mimi ningefurahi kuona kuwa hii ni BBT ya malisho," alisema Mhe. Balozi Dkt. Bashiru.

Aidha, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru amehimiza wafugaji kupewa elimu ya uzalishaji wa malisho na kuagiza utekelezaji wa programu hiyo uishirikishe Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana ili kuwafikia vijana wengi zaidi.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa BBT kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mkurugenzi wa Tathmini na Ufuatiliaji, Dkt. Daudi Mayeji amesema kuwa wizara hiyo imetengewa dola za Marekani milioni 32.8 sawa na shilingi bilioni 81 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo, huku uwekezaji wa awali wa Kituo cha Kongwa ukiwa dola milioni 11.82.

Programu ya BBT ilianza mwaka 2018 kupitia TALIRI kwa kushirikiana na PASS Trust Tanzania, ikilenga kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia mnyororo wa thamani wa mifugo na kuchangia uchumi wa taifa.

# MATUKIO KWENYE PICHA

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali uliofanywa na viongozi na wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwezi Januari, 2026











Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Wizara ya Mifugo Na Uvuvi




**Kwa mawasiliano zaidi:**

Kingolwira (Morogoro) - 0787493792
Mwamapuli (Tabora) - 0779154377
Ruhila (Songea) - 0659669227

www.mifugouvuvi.go.tz

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi